


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA SITA



**25 APRILI, 2019**

## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 25 APRILI, 2019**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**132. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mkoa wa Dodoma una upungufu wa Walimu 527 wa Sayansi:-

Je, ni lini Serikali italeta Walimu wa kutosha wa Sayansi.

**133. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENAN  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini Serikali inatenga na kutumia fedha kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO:**

**134. MHESHIMIWA MAHMOUD HASSAN MGIMWA  
(MUFINDI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Kinyanambo A – Isalavamu – Igombavanu – Sadani hadi Madibira ilikuwepo kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010 na 2010 – 2015

lakini hadi sasa haijajengwa kwa kiwango cha lami:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizofanya Serikali kutoanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wa Wilaya za Mbarali na Mufindi;
- (b) Je, ni lini sasa ujenzi wa Barabara hiyo utaanza;
- (c) Je, ni lini Serikali itaanza uthamini kwa ajili ya kuwalipa fidia Wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara hiyo.

#### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

#### **135. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Vitendo vya Utekaji kwa watu wasio na hatia na kuwatesa, kuwahujumu na hata kuwaua vinaendelea kukithiri nchini:-

- (a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia, kulinda na kuhakikisha inakomesha vitendo hivyo haraka;

(b) Je, hadi sasa ni watu wangapi ambao wamekamatwa na kuchukuliwa hatua kutokana na uhalifu huo.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **136. MHESHIMIWA GOODLUCK ASAPH MLINGA (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wilaya ya Ulanga ina Shule za Msingi zaidi ya 50 na Sekondari zaidi ya 17 lakini haina Chuo chochote ambacho Wanafunzi wanaomaliza masomo kwenye Shule hizo wanaweza kujunga:-

Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo.

## **V. KAULI ZA MAWAZIRI:**

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

## **VI. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**(Majadiliano yanaendelea)**

**DODOMA**  
**25 APRILI, 2019**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**